JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU

BARAZA LA TAIFA LA BIASHARA

# MWONGOZO WA MAJADILIANO KATI YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI NGAZI YA MIKOA NA WILAYA



2020


LA TAIFA LA BIASHARA
O WA KUMI NA MOJA WA BARAZA















# YALIYOMO


Orodha ya Vifupisho....vii

Neno la Waziri.... viii

**SURA YA KWANZA....1**

UTANGULIZI....1

1.1. Lengo la Mwongozo .... 1

1.2. Kuandaa Mwongozo.... 1

1.3. Walengwa wa Mwongozo .... 2

**SURA YA PILI....3**

TAFSIRI YA MANENO MUHIMU.... 3

2.1. Majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi .... 3

2.2. Baraza la Biashara .... 3

2.3. Washiriki .... 3

2.3.1. Wajumbe.... 3

2.3.2. Waalikwa.... 3

2.3.3. Waratibu .... 4

2.3.4. Vinara wa Majadiliano .... 4

2.3.5. Washirika wa Maendeleo .... 5

2.4. Majukumu ya Taasisi mbalimbali Kwa Baraza la Biashara la Mkoa au Wilaya .... 5

2.4.1. Baraza la Taifa la Biashara .... 5

2.4.2. Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ............ 6

2.4.3. Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania ...................................... 7

**SURA YA TATU...................................................................................8**

MWONGOZO.............................................................................................8

3.1. Muundo wa Baraza la Biashara........................ .................. .......8

3.1.1. Baraza........... ..................................................................... 8

3.1.2. Kamati Tendaji.................................................................... 9

3.1.3. Kamati za Baraza ............................................................. 11

3.1.4. Sekretarieti........................................................................ 11

3.2. Maandalizi ya Majadiliano ........................................................ 12

3.2.1. Kuandaa Ajenda................................................................ 12

3.2.2. Wito wa Mkutano ............................................................. 13

3.3. Taratibu za Majadiliano ............................................................ 14

3.3.1. Jukumu la Mwenyekiti ...................................................... 14

3.3.2. Ushiriki na Wajibu wa Wajumbe....................................... 14

3.3.3. Washiriki wa Mikutano ..................................................... 15

3.3.4. Wataalamu na Washauri Waelekezi ................................. 17

3.3.5. Akidi ya Mkutano.............................................................. 17

3.3.6. Mfumo wa Ukaaji ............................................................. 17

3.3.7. Majumuisho na Muhtasari wa Majadiliano...................... 18

3.4. Utekelezaji na Ufuatiliaji wa Maazimio ..................................... 18

3.4.1. Muhtasari wa Majadiliano. ............................................ 18

3.4.2. Ufuatiliaji na Tathmini .................................................... 19

3.4.3. Usambazaji wa Taarifa..................................................... 19

3.4.4. Uhusiano kati ya DBCs, RBCs na TNBC ............................ 20

3.5. Idadi ya Mikutano ya Baraza la Biashara la Mkoa na Wilaya...... 20

**SURA YA NNE................................................................................ 21**

BAJETI ZA KUENDESHA RBCs NA DBCs. ............................................. 21

4.1. Mkutano wa Baraza.................................................................. 21

4.2. Mkutano wa Kamati Tendaji...................................................... 21

**SURA YA TANO.............................................................................. 22**

VIAMBATISHO..........................................................................22

Kiambatisho Na. 1

Uteuzi wa Wajumbe wa Baraza na Kamati Tendaji ............................ 22

Wajumbe wa Baraza kutoka Sekta ya Umma ..................................... 22

Wajumbe wa Baraza kutoka Sekta Binafsi .......................................... 22

Wajumbe wa Kamati Tendaji ............................................................. 23

Kiambatisho Na. 2

Kazi na Majukumu ya Kamati za Baraza................................................24

Kiambatisho Na. 3

Kazi na Majukumu ya Sekretarieti ya Baraza la Biashara .................... 25

Kiambatisho Na. 4

Mambo ya kuepuka kwa Washiriki .................................................. 26

Kiambatisho Na. 5

Mifano ya kazi za Wataalamu/washauri waelekezi ............................. 28

Kiambatisho Na. 6

Mfano wa Sababu zinazoweza kupelekea kuahirishwa kwa Mkutano wa Baraza.........................................................................30

Kiambatisho Na. 7

Mfano wa Bango kitita la utekelezaji wa Maazimio ya Mikutano.........31

Kiambatisho Na. 8a

Mfano wa Bajeti ya mkutano wa Baraza la Biashara la Wilaya.............32

Kiambatisho Na. 8b

Mfano wa bajeti ya Baraza la Biashara la Mkoa...................................32

# ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| ACT | Baraza la Kilimo Tanzania |
| CTI | Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania |
| DANIDA | *Danish International Development Agency* |
| DBC | Baraza la Biashara la Wilaya |
| DED | Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa |
| ENGINE | *Enabling Growth Through Investment and Enterprise* |
| JWT | Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania |
| LIC | *Local Investment Climate Project* |
| OR-TAMISEMI | Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| OWM | Ofisi ya Waziri Mkuu |
| PPD | Majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi |
| PPP | Ushirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi |
| RAS | Katibu Tawala wa Mkoa |
| RBC | Baraza la Biashara la Mkoa |
| LATRA | Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini |
| TAHA | *Tanzania Horticulture Association* |
| TARURA | Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini |
| TBS | Shirika la Viwango Tanzania |
| TCCIA | Chemba ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Wakulima Tanzania |
| TMDA | Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba |
| TNBC | Baraza la Taifa la Biashara |
| TPSF | Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania |
| TRA | Mamlaka ya Mapato Tanzania |
| USAID | *United States Agency for International Development* |

# NENO LA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU - SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU




Tanzania inatambua kuwa Sekta Binafsi ni chachu ya ukuaji wa uchumi wa Taifa. Kwa kutambua hilo, Serikali imeamua kuchukua hatua za makusudi ili kuchochea ushiriki na shughuli za Sekta Binafsi kwa kufanya maboresho muhimu ya Sera, Sheria, Miongozo na Kanuni mbalimbali zinazosimamia Sekta Binafsi. Maboresho hayo yanalenga kujenga mazingira rafiki na wezeshi ya kufanya biashara na kuvutia uwekezaji. Sekta Binafsi inapoimarika na kuwa shindani inatarajiwa kuchochea maendeleo ya Nchi kupitia makusanyo ya kodi mbalimbali na kuzalisha fursa za ajira.

Serikali imeandaa Mwongozo huu wa majadiliano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kupitia Mabaraza ya Biashara katika ngazi za Mikoa na Wilaya ili kuweka misingi bora ya majadiliano ili kujenga uelewa na mtazamo wa pamoja kuhusu masuala muhimu ya maendeleo kati ya Sekta hizi mbili. Utekelezaji wa Mwongozo huu utapelekea uwepo wa mazingira wezeshi kibiashara, utajenga kuaminiana miongoni mwa wadau na hivyo kuifanya Sekta Binafsi kuwa endelevu.

Mwongozo huu unatarajia kuimarisha ushiriki wa Sekta Binafsi katika kutekeleza mipango ya maendeleo ya Nchi katika masuala yanayohusu

maendeleo ya biashara na uwekezaji. Mwongozo utajenga uelewa miongoni mwa Wadau juu ya majukumu ya msingi yanayotekelezwa na Sekta ya Umma hususani ujenzi wa mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji kufikia Uchumi wa Kati kupitia Viwanda ifikapo mwaka 2025.

Ni matumaini yangu kuwa wale wote wanaohusika kama wadau wakuu wa shughuli za majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kupitia Mabaraza ya Biashara ya Mikoa na Wilaya watatekeleza majukumu yao ipasavyo na kwa kuzingatia Mwongozo huu. Hivyo, nitoe wito kwa Taasisi za Umma, Sekta Binafsi na Wadau wengine katika maendeleo ya biashara na uwekezaji wazingatie Mwongozo huu kikamilifu. Hili ni jambo muhimu sana katika kuhakikisha kuwa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wanashirikiana ipasavyo katika kuhakikisha Nchi yetu inafikia Uchumi wa Kati.



Jenista J. Mhagama (Mb)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU - SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU**

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1. Lengo la Mwongozo

Mwongozo unalenga kujenga uwezo wa Mabaraza ya Biashara ya Mikoa na Wilaya kwa kuelezea taratibu muhimu za kuzingatia katika kuendesha majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ili yaweze kuwa endelevu na yenye tija katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, kuchochea ukuaji wa uchumi na maendeleo ya Taifa. Ili Majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi yawe na tija yanapaswa kuzingatia mambo yafuatayo:

i. Muundo na Washiriki
ii. Maandalizi ya majadiliano
iii. Taratibu za majadiliano
iv. Utekelezaji na Ufuatiliaji wa maazimio

Viambatisho vinavyotoa maelezo zaidi pamoja na mifano mbalimbali kama bajeti, mambo ya *kufanya au kuepuka,* vimewekwa katika mwongozo huu.

## 1.2. Kuandaa Mwongozo

Mbinu shirikishi zilitumika katika kuandaa Mwongozo huu. Wadau wakuu walishirikishwa na kushiriki katika kutoa maoni kuhusu Mwongozo. Wadau hao ni wale wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

## 1.3 Walengwa wa Mwongozo

Walengwa wa mwongozo huu ni wadau wa Majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ikiwemo Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Ofisi za Wakuu wa Wilaya, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi za Umma, Taasisi za Sekta Binafsi, Viongozi na Wawakilishi wa Sekta Binafsi, Wafanyabiashara na Wawekezaji, Asasi za Kiraia na Wadau wa Maendeleo.

# SURA YA PILI

## TAFSIRI YA MANENO MUHIMU

### 2.1. Majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

Ni mkutano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wenye lengo la kufikia makubaliano na uelewa wa pamoja kuhusu masuala ya kimkakati yanayolenga kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Katika Mwongozo huu neno "Majadiliano" limetumika sawa na neno "Majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi".

### 2.2. Baraza la Biashara

Baraza la Biashara ni jukwaa rasmi la Majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi katika ngazi ya Taifa, Mkoa na Wilaya.

### 2.3. Washiriki

Washiriki wa Majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wanatokana na makundi yafuatayo:-

#### 2.3.1. Wajumbe

Wajumbe wa majadiliano ni wale walioteuliwa kwa barua na mwenyekiti wa Baraza katika ngazi husika.

#### 2.3.2. Waalikwa

Mbali na wajumbe wa Baraza la Biashara la Mkoa au Wilaya, kulingana na ajenda, wawakilishi wa Sekta ya Umma, Sekta Binafsi na makundi ya kiraia wanaweza kualikwa kwenye mkutano. Lengo ni kuongeza wigo wa ushiriki na kupata maoni na mapendekezo zaidi kuhusu ajenda za mkutano.

Kwa kutambua umuhimu wa Wenyeviti wa Halmashauri, Meya wa Manispaa na Wenyeviti wa Kamati ndogo za Halmashauri katika kuwezesha utekelezaji wa maazimio ya majadiliano, Mwongozo unaelekeza wawe sehemu ya waalikwa kwenye mikutano ya Baraza la Biashara.

### 2.3.3. Waratibu

Katika ngazi ya Mkoa, Baraza la Biashara linaratibiwa na ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa na katika ngazi ya Wilaya linaratibiwa na ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri/ Manispaa/Jiji. Ofisi ya Katibu Tawala ya Wilaya itaratibu shughuli za Baraza la Biashara la Wilaya pale ambapo Wilaya ina Halmashauri zaidi ya moja kwa kuwashirikisha Wakurugenzi wa Halmashauri zote. Izingatiwe kuwa, Baraza la Biashara ni la Wilaya na si Halmashauri. Katika ngazi zote, uratibu wa shughuli za Baraza la Biashara utafanyika kwa kushirikiana na Sekta Binafsi.

### 2.3.4. Vinara wa majadiliano

Vinara au wahamasishaji ni watu muhimu katika kuwezesha Majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kufanyika na kuwa endelevu. Vinara wanao wajibu wa kuhamasisha wadau kuhusu umuhimu wa majadiliano na wanaweza kutoka Sekta ya Umma au Sekta Binafsi, Wanasiasa na Wataalam.

Rais wa nchi ndiye kinara wa Majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kupitia Baraza la Taifa la Biashara. Katika ngazi za Mkoa na Wilaya, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wanategemewa kuwa vinara muhimu wa Mabaraza ya Biashara. Kwa upande wa Sekta Binafsi, viongozi wa taasisi za Sekta Binafsi wanategemewa kuchukua jukumu la kuongoza na kuwa vinara wa majadiliano.

#### 2.3.5. Washirika wa maendeleo

Washirika wa maendeleo wanaweza kualikwa kuchangia sehemu ya gharama au gharama zote za uratibu wa Mabaraza ya Biashara. Hata hivyo Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri za Wilaya zinaelekezwa kutenga bajeti ili kupunguza utegemezi wa Washirika wa Maendeleo.

### 2.4. Majukumu ya Taasisi mbalimbali Kwa Baraza la Biashara la Mkoa/Wilaya

#### 2.4.1. Baraza la Taifa la Biashara

i. Kutoa miongozo mbalimbali ya kuimarisha ufanisi wa majadiliano.
ii. Kujengea uwezo Mabaraza ya Biashara ya Mikoa na Wilaya.
iii. Kuwa kiunganishi kati ya Taasisi za Serikali katika ngazi ya Taifa, Sekretarieti za Mikoa, Wilaya na Mamlaka za Serikali za Mitaa, kwenye utekelezaji wa maazimio yanayotokana na majadiliano.

iv. Kuweka taarifa na maazimio ya Mabaraza ya Biashara ya Mkoa/Wilaya katika tovuti ya Baraza la Taifa la Biashara.
v. Kuhakikisha taarifa na mapendekezo yanayotokana na Mabaraza ya Biashara ya Mkoa/Wilaya yanayohitaji maamuzi ngazi ya Taifa, yanawasilishwa kwenye mkutano wa Baraza la Taifa la Biashara.
vi. Kusaidia Mabaraza ya Biashara kufanya tafiti mbalimbali za kisera na kufanya ufuatiliaji na tathmini.
vii. Kutoa taarifa ya maazimio yaliyofikiwa katika mikutano ya Baraza la Taifa la Biashara pamoja na maelekezo mengine kwa Baraza la Biashara la Mkoa kama itakavyoonekana inafaa.
viii. Kusaidia Mkoa na Wilaya katika kuhabarisha kuhusu mafanikio yaliyopatikana katika mazingira ya biashara na uwekezaji kwa wadau mbalimbali na umma.

**2.4.2. Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.**

i. Kusimamia na kufuatilia utendaji wa Mabaraza ya Biashara ya Mkoa na Wilaya.
ii. Kufuatilia utekelezaji wa maazimio ya Mabaraza ya Biashara ya Mkoa na Wilaya
iii. Kuwa kiunganishi kati ya Mabaraza ya Biashara ya Mkoa na Wilaya na wadau wengine.
iv. Kuhakikisha Sekretarieti ya Mkoa na Halmashauri zinatenga Bajeti ya uratibu wa Mabaraza ya Biashara.

### 2.4.3. Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania

i. Kuimarisha vyama vya kibiashara katika ngazi ya Mkoa na Wilaya.

ii. Kuratibu majadiliano miongoni mwa Sekta Binafsi ili kuongeza ufanisi wa majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

# SURA YA TATU

# MWONGOZO

## 3.1. Muundo wa Baraza la Biashara

Majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kupitia Baraza la Biashara yataendeshwa na vyombo vifuatavyo;

- Baraza
- Kamati Tendaji
- Kamati za Baraza
- Sekretarieti

### 3.1.1. Baraza

i. Mwenyekiti wa Baraza la Biashara la Mkoa ni Mkuu wa Mkoa.

ii. Mwenyekiti wa Baraza la Biashara la Wilaya ni Mkuu wa Wilaya.

iii. Baraza la Biashara la Mkoa na Wilaya litakuwa na wajumbe 40 kila moja. Wajumbe 20 watatoka Sekta ya Umma, ambao watateuliwa kutokana na nafasi walizonazo Serikalini, ambazo ni Katibu Tawala wa Mkoa, Wakuu wa Wilaya na watendaji wakuu wa Taasisi za Umma kutoka sekta muhimu za kiuchumi.

iv. Wajumbe 20 wengine watatoka Sekta Binafsi, ambao watapendekezwa na Sekta Binafsi kupitia TCCIA kwa kuzingatia uwakilishi wa sekta za kiuchumi, vyama vya kibiashara, kundi la vijana na wanawake kwa kufuata mwongozo kutoka Taasisi ya Sekta Binafsi ya Tanzania

(TPSF) na kwa kushirikisha sekta husika. Wajumbe watateuliwa kwa kipindi cha miaka mitatu.

v. Katika Wilaya zenye Halmashauri zaidi ya moja, uteuzi wa wajumbe wa Baraza kwa upande wa Sekta ya Umma utafanywa na Mwenyekiti wa Baraza la Biashara kwa kuwashirikisha Wakurugenzi wa Halmashauri zote.

*Zingatio:* Mwenyekiti wa Baraza la Biashara hana mwenyekiti mwenza

*Tazama Kiambatisho namba 1*: Uteuzi wa wajumbe wa Baraza na Kamati Tendaji

### 3.1.2. Kamati Tendaji

Kamati Tendaji ya Baraza ina jukumu la kusimamia shughuli za kila siku za Baraza. Kamati Tendaji inaongozwa na Mwenyekiti pamoja na Mwenyekiti Mwenza.

i. Mwenyekiti wa Kamati Tendaji ya Mkoa ni Katibu Tawala wa Mkoa na Mwenyekiti mwenza ni Kiongozi wa TCCIA ngazi ya Mkoa akiwakilisha Sekta Binafsi.

ii. Mwenyekiti wa Kamati Tendaji ya Wilaya ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, na Mwenyekiti mwenza ni Kiongozi wa TCCIA ngazi ya Wilaya akiwakilisha Sekta Binafsi.

iii. Muundo wa sasa una wajumbe kumi (10), wajumbe watano (5) kutoka Sekta Binafsi na watano (5) kutoka sekta ya umma. Idadi ya wajumbe wa Kamati Tendaji inaweza kuongezeka kulingana na mahitaji ya Mkoa au Wilaya husika.

iv. Wajumbe kutoka Sekta ya Umma ngazi ya Mkoa watakuwa Wakuu wa Idara zifuatazo; Idara ya Uchumi na Uzalishaji; Idara ya Mipango na Uratibu; Idara ya Ujenzi; Idara ya Ardhi; na Wakuu wa Taasisi za Udhibiti, kama vile TMDA, TBS, n.k. Kwa ngazi ya Wilaya watakuwa Wakuu wa idara na Wakuu wa Taasisi za umma kama vile; Idara ya Kilimo; Idara ya Mipango; Idara ya Miundombinu (TARURA); Idara ya Ardhi; na Mweka hazina wa Wilaya.
v. Wajumbe kutoka Sekta Binafsi inapendekezwa watoke miongoni mwa wajumbe wa Baraza la Biashara.

#### 3.1.2.1. Majukumu ya Kamati Tendaji

i. Kuandaa ajenda za mkutano wa Baraza la Biashara.
ii. Pia Kamati ina wajibu wa kuchambua, kujadili na kutatua changamoto zilizo ndani ya mamlaka yake.
iii. Kusimamia utekelezaji wa maamuzi ya Baraza na kutoa mrejesho kwa Baraza na wadau wengine.

#### 3.1.2.2. Wilaya yenye Halmashauri zaidi ya moja

i. Wajumbe wa Sekta ya Umma watatoka kwenye Halmashauri zote ikijumuisha Wakurugenzi wa Halmashauri pamoja na Wakuu wa Idara toka Halmashauri zote kwa uwiano utakaokubaliwa na Wakurugenzi.
ii. Katibu Tawala wa Wilaya ndiye atakuwa

Mwenyekiti na Ofisi yake ndio itaratibu shughuli za Baraza la Biashara.

iii. Katika mazingira haya, idadi ya wajumbe inaweza kuongezeka kulingana na mahitaji ya Wilaya husika na kwa kuzingatia uwiano sawa kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.
*Tazama Kiambatisho namba 1: Uteuzi wa wajumbe wa Baraza na Kamati Tendaji.*

### 3.1.3. Kamati za Baraza

Katika kutekeleza majukumu yake, Baraza la Biashara linaweza kuanzisha kamati za kudumu au za muda kufanyia kazi fursa au changamoto mbalimbali. Kamati zitakazoundwa zitafanya kazi na kutoa mapendekezo kupitia Kamati Tendaji. Kamati hizi zinaweza kuundwa kwa mfumo wa kongano, kikundi kazi au kikosi kazi.
*Tazama Kiambatisho namba 2: Kazi na majukumu ya Kamati za Baraza.*

### 3.1.4. Sekretarieti

Baraza litakuwa na Sekretariati kwa ajili ya kuratibu shughuli zote, ikiwa ni pamoja na kuisaidia Kamati Tendaji kutekeleza majukumu yake.

i. Sekretarieti inaundwa na Afisa Biashara wa Mkoa au Wilaya. Afisa Mtendaji wa TCCIA Mkoa au Wilaya ataiwakilisha Sekta Binafsi katika Sekretarieti ya Baraza la Biashara la Mkoa au Wilaya.

ii. Pale ambapo kuna Halmashauri zaidi ya moja,

Sekretarieti ya Baraza la Biashara itaundwa na wajumbe kutoka Halmashauri zote; ikiwa ni Maafisa Biashara pamoja na wawakilishi kutoka Sekta Binafsi kwa uwiano sawa. Sambamba na Sekretarieti, Afisa Biashara atakuwa Katibu wa Kamati Tendaji.

*Kiambatisho namba 3: Kazi na majukumu ya Sekretarieti*

## 3.2. Maandalizi ya Majadiliano

### 3.2.1. Kuandaa Ajenda

Mchakato wa kuandaa ajenda za Mikutano unashauriwa kuanza kwa kila sekta kufanya majadiliano na wadau wake kupitia njia zifuatazo:

i. Majadiliano ndani ya Sekta Binafsi yenye lengo la kuimarisha uelewa na makubaliano ya pamoja kuhusu ajenda zitakazojadiliwa kwenye Mikutano ya Mabaraza ya Biashara.




ii. Majadiliano ndani ya Sekta ya Umma katika ngazi ya Mkoa na Wilaya kwa lengo la kuimarisha uelewa na makubaliano ya pamoja kuhusu ajenda zitakazojadiliwa kwenye Mikutano ya Mabaraza ya Biashara.

iii. Pia ajenda za majadiliano zinaweza kutokana na majadiliano ya kisekta na mikutano ya kisheria ya

kuwasilisha kero na fursa katika ngazi za Kata, Wilaya na Mkoa au Tasisi mbalimbali ambazo zimefanyika.

iv. Kamati Tendaji itajadili na kupitisha ajenda za Mkutano wa Baraza la Biashara. Pale ambapo itaonekana kuna uhitaji wa utafiti/taarifa zaidi, Mshauri Mwelekezi anaweza kutumika.

v. Kipaumbele cha ajenda ya Mkutano wa Baraza la Biashara ni kujadili masuala yatakayoimarisha maendeleo ya uchumi wa Wilaya au Mkoa husika au masuala yanayoweza kupatiwa ufumbuzi na Mamlaka za Wilaya na Mkoa,

vi. Pia, Baraza la Biashara litajadili fursa za utekelezaji wa miradi midogo ya ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*Small Scale PPP Projects*) katika ngazi za Halmashauri.

### 3.2.2. Wito wa Mkutano

Mwenyekiti wa Baraza la Biashara atawajulisha kwa barua ya wito wa Mkutano, wajumbe pamoja na waalikwa kuhusu Mkutano wa Baraza wiki mbili kabla ya mkutano. Washiriki wanapaswa kuthibitisha ushiriki wao wiki moja kabla ya Mkutano. Barua ya wito itaambatana na makabrasha ya Mkutano.

## 3.3. Taratibu za Majadiliano

### 3.3.1. Jukumu la Mwenyekiti

i. Kuongoza majadiliano ili kufikia maridhiano.
ii. Anapaswa kutofungamana na upande wowote miongoni mwa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.
iii. Ikiwa Mwenyekiti ana ajenda ya kuwasilisha katika Mkutano wa Baraza, ni vema ajenda hiyo ikawasilishwa kupitia Kamati Tendaji.
iv. Mwenyekiti anatakiwa kuwepo wakati wote, ili majadiliano yaweze kuwa na ufanisi. Ni jukumu la Mwenyekiti kuhakikisha Mkutano wa Baraza la Biashara unafanyika kwa wakati.

### 3.3.2. Ushiriki na Wajibu wa Wajumbe

i. Washiriki wote wanapaswa kuhudhuria Mkutano wakiwa wamejiandaa na kushiriki katika majadiliano kwa kutoa maoni, mapendekezo, uzoefu, uelewa au maelezo zaidi kuhusu ajenda ya majadiliano. Washiriki wajielekeze zaidi kujadili suluhu ya jambo linalojadiliwa.
ii. Kusikiliza na kuelewa jambo kabla ya kuzungumza; kuzungumza kwa staha na hekima na kuzingatia muda ili kutoa nafasi kwa washiriki wote kuweza kuchangia.
iii. Kuhudhuria Mikutano bila kukosa na kuwepo kwenye majadiliano kwa muda wote.
iv. Kuhamasisha utekelezaji wa makubaliano yaliyofikiwa katika Mikutano ya Baraza na kuwa Balozi wa kuhabarisha kuhusu matokeo chanya ya Mabaraza, kwa kundi analoliwakilisha na Umma kwa ujumla.

v. Wajumbe wanapaswa kutoa mrejesho kwa kundi analoliwakilisha kuhusu maazimio ya Mikutano na hatua zinazochukuliwa kutekeleza maazimio hayo.
*Tazama Kiambatisho namba 4: Mambo ya kuepuka kwa washiriki*

### 3.3.3. Washiriki wa Mikutano

Washiriki wa Majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wanatokana na makundi yafuatayo:

#### 3.3.3.1. Wajumbe

Wajumbe wa majadiliano ni wale walioteuliwa kwa barua na Mwenyekiti wa Baraza katika ngazi husika.

**(a) Wajumbe wa Baraza kutoka sekta ya umma**

Kwa ngazi ya Mkoa watatoka makundi yafuatayo:

i. Katibu Tawala wa Mkoa (RAS),
ii. Wakuu wa Wilaya,
iii. Watendaji Wakuu wa Taasisi za Umma kama vile TANESCO, Mamlaka za Maji, TRA, TBS, TMDA, LATRA, Polisi, Uhamiaji (Hasa mikoa ya mpakani) na OSHA.

Kwa ngazi ya Wilaya watatoka makundi yafuatayo:

i. Katibu Tawala wa Wilaya (DAS),
ii. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri. Pale ambapo kuna Halmashauri zaidi ya moja,

Wakurugenzi wa Halmashuri zote watakuwa Wajumbe wa Baraza

iii. Watendaji Wakuu wa Taasisi za Umma kama vile TANESCO, Mamlaka za Maji, TRA, TBS, TMDA, LATRA, Polisi, Uhamiaji (Hasa mikoa ya mpakani) na OSHA.

**(b) Wajumbe wa Baraza kutoka Sekta Binafsi**

Wajumbe wa Sekta Binafsi kwa ngazi ya Mkoa na Wilaya watapendekezwa na Sekta Binafsi kwa kuzingatia mambo yafuatayo:

i. Uwakilishi wa sekta za kiuchumi kama vile kilimo, Uvuvi, Mifugo, Madini, Utalii, Biashara, Fedha, Huduma, Ujenzi, Usafirishaji, na Viwanda.

ii. Uwakilishi kutoka makundi muhimu kama vile Wanawake, Vijana na Sekta Isiyo Rasmi

iii. Uwakilishi wa Taasisi za Sekta Binafsi kama vile TCCIA, JWT, ACT, TAHA na CTI.

iv. Wafanyabiashara wadogo, wakati na wakubwa.

**3.3.3.2. Waalikwa**

Mbali na wajumbe wa Baraza la Biashara la Mkoa au Wilaya, kulingana na ajenda, wawakilishi wa Sekta ya Umma, Sekta Binafsi na makundi ya kiraia wanaweza kualikwa kwenye Mkutano. Lengo ni kuongeza wigo wa ushiriki na kupata maoni na mapendekezo zaidi kuhusu ajenda za mkutano.

### 3.3.4. Wataalamu na Washauri Waelekezi

Wataalamu na Washauri Waelekezi wanaweza kutumika kwenye mambo yafuatayo:

i. Kutoa ushauri au maoni juu ya ajenda za Mkutano.
ii. Kufanya tafiti au maandiko mbalimbali kwa ajili ya majadiliano.
iii. Kuwasilisha mada fupi kwenye Mkutano wa Baraza la Biashara.

*Tazama Kiambatisho namba 5: Mifano ya kazi za Wataalam na Washauri Waelekezi.*

### 3.3.5. Akidi ya Mkutano

i. Akidi ya Mkutano wa Baraza la Biashara inapaswa kulenga katika kufikia maridhiano na idadi isiyopungua nusu ya wajumbe wote na kila upande ukiwa na wajumbe wasiopungua wanane.
ii. Akidi ya Mkutano wa Kamati Tendaji ya Baraza inapaswa kutopungua nusu ya wajumbe wote na kila upande ukiwa na wajumbe wasiopungua wawili

*Tazama kiambatisho namba 6: Sababu za kuahirishwa kwa Mkutano wa Baraza*

### 3.3.6. Mfumo wa Ukaaji

i. Mfumo wa ukaaji wa mzunguko au umbo la “U” utatumika katika majadiliano kupitia Mikutano na vikao vya Baraza la Biashara.
ii. Dhumuni ni kujenga hali ya ushirikiano, umoja na usawa katika majadiliano. Pia ukaaji unapaswa kuchanganya wajumbe wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

iii. Mbali na mfumo wa ukaaji, wajumbe wanatakiwa kutambua dhana ya jukwaa moja na mjadala mmoja wakati wote wa majadiliano katika Mikutano na Vikao vya Baraza la Biashara

**Mfano**



*Picha: Mfumo wa ukaaji wa umbo "U"*

### 3.3.7. Majumuisho na Muhtasari wa Majadiliano

Sekretarieti ya Baraza itaandaa muhtasari wa maazimio ya mkutano wa Baraza la Biashara ambao utasomwa na Katibu wa Baraza kabla ya Mwenyekiti kuahirisha majadiliano.

## 3.4. Utekelezaji na Ufuatiliaji wa Maazimio

### 3.4.1. Muhtasari wa Majadiliano.

Sekretarieti itaandaa rasimu ya muhtasari wa majadiliano, maazimio na bango kitita la utekelezaji na kuwasilisha kwa wajumbe wa Baraza ndani ya wiki moja baada ya mkutano. Wajumbe wanapaswa kuwasilisha maoni yao na maboresho ndani ya siku tano baada ya kupokea rasimu ya muhtasari wa Mkutano.

*Tazama Kiambatisho namba 7 Mfano wa Bango kitita la utekelezaji wa maazimio ya mkutano.*

### 3.4.2. Ufuatiliaji na Tathmini

Kamati Tendaji itaunda kamati maalum ya kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa maazimio ya majadiliano na kutoa taarifa. Ufanisi wa majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi unaweza kupimwa kwa kutumia viashiria mbalimbali ikiwa ni pamoja na matokeo ya majadiliano, utekelezaji wa maazimio, ushiriki na uwakilishi wa wajumbe. Taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya Mkutano au kikao kilichopita itawasilishwa katika kikao kabla ya kujadili ajenda mpya na taarifa hiyo itatambulika kama "yatokanayo na Kikao/Mkutano husika".

### 3.4.3. Usambazaji wa Taarifa

Matokeo na mafanikio ya majadiliano yanapaswa kusambazwa kwa wadau muhimu na umma kwa ujumla. Vyombo vya habari ni muhimu kwa ajili ya kufahamisha umma kuhusu majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kwa misingi ya uwazi na uwajibikaji. Kamati Tendaji itaamua uwepo wa vyombo vya habari wakati wa majadiliano kama itakavyoona inafaa. Hata hivyo Mikutano na waandishi wa habari pamoja na taarifa kwa vyombo vya habari vitaandaliwa na kusambazwa na Kamati Tendaji ili kufahamisha umma.

Katibu Tawala Mkoa atakuwa na jukumu la kuwasilisha Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, taarifa na matokeo ya Mikutano ya Mabaraza ya Biashara ya Mkoa na

Wilaya kila robo ya mwaka na nakala kupelekwa Baraza la Taifa la Biashara.

### 3.4.4. Uhusiano kati ya DBCs, RBCs na TNBC

Ajenda zinazohitaji mjadala katika ngazi ya Mkoa pamoja na mafanikio ya Mabaraza ya Biashara kwa ngazi ya Wilaya zitawasilishwa Baraza la Biashara la Mkoa kupitia Kamati Tendaji. Ajenda zinazohitaji mjadala katika ngazi ya Taifa pamoja na mafanikio ya Mabaraza ya Biashara ya Mkoa zitawasilishwa Baraza la Taifa la Biashara kupitia Sekretarieti ya Baraza la Taifa la Biashara. Kutoa taarifa ya maazimio yaliyofikiwa katika Mikutano ya Baraza la Taifa la Biashara pamoja na maelekezo mengine kwa Baraza la Biashara la Mkoa kama itakavyoonekana inafaa.

## 3.5. Idadi ya Mikutano ya Baraza la Biashara la Mkoa na Wilaya

Baraza la Biashara la Mkoa au Wilaya linapaswa kukutana angalau mara mbili kwa mwaka. Hata hivyo, linaweza kukutana zaidi kulingana na uhitaji.

# SURA YA NNE

# BAJETI ZA KUENDESHA RBCs NA DBCs.

Kazi za Mabaraza ya Biashara zitagharamiwa kwa mfumo wa uchangiaji kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kwa uwiano sawa wa asilimia hamsini kwa hamsini. Sekretarieti ya Mkoa na Halmashauri ya Wilaya itatenga bajeti ya kugharamia kazi za Baraza la Biashara. Sekta Binafsi itagharamia kupitia vyama vyao. Pia misaada mingine ya fedha taslim au udhamini inaweza kutoka kwa Sekta Binafsi, Wahisani na Washirika wa Maendeleo.

## 4.1. Mkutano wa Baraza

Gharama za Mikutano ya Mabaraza ya Biashara ya Mikoa na Wilaya zinatokana na vipengele vifuatavyo; Gharama za shajala; viburudisho (chakula na maji); gharama za ukumbi; na gharama za mawasiliano na taarifa za mialiko. Gharama zinaweza kuongezeka kulingana na mahitaji, kama vile kumpata mshauri mwelekezi

*Kiambatisho namba 8a na 8b kinaonyesha mfano wa bajeti ya Mkutano wa Baraza la Biashara la Mkoa na Wilaya.*

## 4.2. Mkutano wa Kamati Tendaji

Gharama za Kikao cha Kamati Tendaji ya Baraza la Biashara la Mkoa na Wilaya zinatokana na vipengele vifuatavyo; Gharama za shajala; viburudisho (chakula na maji). Gharama zinaweza kuongezeka kulingana na mahitaji, kama vile kukodisha ukumbi na kumpata mshauri mwelekezi.

*Kiambatisho namba 8a na 8b ni mifano ya bajeti ya Kamati Tendaji ya Baraza la Biashara la Mkoa na Wilaya.*

# SURA YA TANO

# VIAMBATISHO

*Kiambatisho Na. 1*

**Uteuzi wa Wajumbe wa Baraza na Kamati Tendaji**

**A. Wajumbe wa Baraza kutoka Sekta ya Umma**

- Kwa ngazi ya Mkoa watatoka makundi yafuatayo**:**
  i. Katibu Tawala wa Mkoa (RAS)
  ii. Wakuu wa Wilaya
  iii. Watendaji Wakuu wa Taasisi za Umma kama vile TANESCO, Mamlaka za Maji, TRA, TBS, TMDA, LATRA, Polisi, Uhamiaji (Hasa mikoa ya mpakani) na OSHA.
- Kwa ngazi ya Wilaya watatoka makundi yafuatayo:
  i. Katibu Tawala wa Wilaya (DAS)
  ii. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri. Pale ambapo kuna Halmashauri zaidi ya moja, Wakurugenzi wa Halmashuri zote watakuwa Wajumbe wa Baraza
  iii. Watendaji Wakuu wa Taasisi za Umma kama vile TANESCO, Mamlaka za Maji, TRA, TBS, TMDA, LATRA, Polisi, Uhamiaji (Hasa mikoa ya mpakani) na OSHA.

**B. Wajumbe wa Baraza kutoka Sekta Binafsi**

- Wajumbe wa Sekta Binafsi kwa ngazi ya Mkoa na Wilaya watapendekezwa na Sekta Binafsi kwa kuzingatia mambo yafuatayo:
  i. Uwakilishi wa sekta za kiuchumi kama vile kilimo, Uvuvi, Mifugo, Madini, Utalii, Biashara, Fedha, Huduma, Ujenzi, Usafirishaji, na Viwanda.
  ii. Uwakilishi kutoka makundi muhimu kama vile Wanawake,

Vijana na Sekta Isiyo Rasmi

iii. Uwakilishi wa Taasisi za Sekta Binafsi kama vile TCCIA, JWT, ACT, TAHA na CTI.

iv. Wafanyabiashara wadogo, wakati na wakubwa

**C. Wajumbe wa Kamati Tendaji**

- Kwa upande wa Sekta ya Umma, Wajumbe wa Kamati Tendaji ngazi ya Mkoa watakuwa ni Watendaji Wakuu wa Taasisi za Umma na Idara za Serikali kama vile:
  - i. Mkuu wa Idara ya Uchumi na Uzalishaji,
  - ii. Mkuu wa Idara ya Mipango na Uratibu,
  - iii. Mkuu wa Idara ya Ujenzi na Miundombinu,
  - iv. Mkuu wa Idara ya Ardhi,
  - v. Mkuu wa Idara ya Afya na
  - vi. Meneja wa TRA Mkoa.
- Kwa ngazi ya Wilaya watakua ni Wakuu wa Idara na Taasisi za Umma kama vile:-
  - i. Mkuu wa Idara ya kilimo,
  - ii. Mkuu wa Idara ya Mipango,
  - iii. Mkuu wa Idara ya Ujenzi na Miundombinu (TARURA),
  - iv. Mkuu wa Idara ya Ardhi,
  - v. Mkuu wa Idara ya Afya,
  - vi. Mkuu wa Idara ya Fedha na
  - vii. Meneja wa TRA.
- Wajumbe wa Kamati Tendaji kutoka Sekta Binafsi

  Wajumbe kutoka Sekta Binafsi inapendekezwa watoke miongoni mwa wajumbe wa Baraza la Biashara. Mwenyekiti mwenza wa Kamati Tendaji atakua Kiongozi wa TCCIA akiwakilisha Sekta Binafsi.

*Kiambatisho Na. 2*

**Kazi na Majukumu ya Kamati za Baraza**

i. Kufanya tathmini na uchambuzi wa kina ili kupata uelewa wa kutosha kuhusu changamoto, hoja au masuala muhimu yanayohusu sekta kama yalivyowasilishwa au kuibuliwa katika majadiliano mbalimbali miongoni mwa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi na kuainisha maeneo yanayohitaji maboresho na matokeo yanayotarajiwa kutokana na maboresho hayo.

ii. Kuainisha, kupendekeza njia ya utekelezaji wa maboresho yaliyoainishwa, pamoja na mpango kazi na muda halisia wa utekelezaji kwa ajili ya kupima utekelezaji wa maboresho hayo.

iii. Kupendekeza utaratibu wa ufuatiliaji na mfumo wa tathmini.

iv. Kujadili na kukubaliana kuhusu mahitaji ya rasilimali zinazohitajika kutekeleza shughuli zake, ikiwa ni pamoja na rasilimali watu, fedha na rasilimali nyingine ili kufanikisha maboreho hayo kwa kuzingatia viashiria vya muda mfupi, kati na mrefu.

v. Kujadili ajenda za Mikutano ya RBC na DBC, kufuatilia maombi ya Kamati Tendaji ya kufanya tafiti kupitia Sekretarieti na kuandaa taarifa za utekelezaji na maandiko ya maboresho ya kisera na kiutendaji

*Kiambatisho Na. 3*

**Kazi na Majukumu ya Sekretarieti ya Baraza la Biashara.**

i. Kuratibu Mikutano na Vikao vyote vya Baraza la Biashara
ii. Kuandaa makabrasha na taarifa muhimu kwa ajili ya Mikutano na Vikao vya Baraza la Biashara
iii. Kuandika muhtasari wa Mkutano au Kikao cha Baraza la Biashara
iv. Kutoa taarifa ya maazimio na maagizo ya Mikutano au Vikao vya Baraza la Biashara kwa wahusika kwa ajili ya utekelezaji na ufuatiliaji
v. Kuratibu na kufuatilia utendaji wa Kamati za Baraza.
vi. Kuweka kumbukumbu za Mikutano ya Baraza na taarifa za shughuli zote zinazohusu Baraza.

**Mambo ya kuepuka kwa Washiriki**

Wajumbe na washiriki wanapaswa kuepuka mambo yafuatayo:

i. Hofu na wasiwasi

ii. Kujadili au kuwasilisha jambo la maslahi ya kibinafsi wakati wa ushiriki.

iii. Kulaumiana, kushtakiana, au kukosoana wakati wa majadiliano

iv. Ikiwa taratibu zote zitafuatwa Mkutano wa DBC ungekuwa ni wa kujadili mambo ya msingi yenye lengo la kujenga na kupata maazimio yanayotekelezeka

**Mfano na.1** Katika Wilaya ya Bahi huko Dodoma, kulikuwa na mkutano wa DBC na washiriki toka Sekta Binafsi walikuwa wasikilizaji tu na wenye hofu. Washiriki hawakuwasilisha mawazo au mapendekezo ya Sekta Binafsi hata baada ya kusukumwa kufanya hivyo. Kufuatia hali hiyo ilimlazimu Mwenyekiti kuteua Wajumbe wapya kutoka Sekta Binafsi, na kuitisha mkutano wa pili wa DBC.

**Mfano na. 2** Wilaya ya Kongwa ambayo pia ipo Mkoa wa Dodoma, wawakilishi wa Sekta Binafsi katika mkutano wa DBC walikuwa wakiilaumu Serikali kuhusu changamoto za Wilaya hiyo, lakini hawakutoa maoni au mapendekezo ya jinsi ya kuzitatua. Hawakutenda haki kwa Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Sekta ya Umma.

**Mfano na. 3** Wakati wa Mkutano wa DBC katika Manispaa ya Dodoma, baadhi ya wajumbe kutoka Sekta Binafsi walizingatia sana kuwasilisha masuala binafsi. Hawakuwa na utayari wa kusikia upande mwingine, hawakuwa na mtazamo wa manufaa kwa pande zote. Hatimaye wajumbe walibadilishwa na Mwenyekiti wa Baraza. Mengi yaliyowasilishwa yalipaswa kuchambuliwa na kujadiliwa kwenye Vikao vya Sekta Binafsi na baadae kwenye Kamati Tendaji.

**Mifano ya kazi za Wataalamu / Washauri Waelekezi**

i. **Ushuru sahihi wa ushuru wa mazao:**

Ili kuisaidia Kongwa DBC, mradi wa LIC ulimwajiri mtaalam wa mafunzo ya maendeleo kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma kufanya utafiti wa kitaalam na mwongozo wa ushuru wa mazao unaotozwa kwa wakulima na wafanyabiashara. Sekta Binafsi ilikuwa ikilalamika juu ya utitiri wa kodi, hivyo Serikali ikapokea utafiti huo. Mtaalamu alifanya utafiti na kupendekeza viwango sahihi vya kutoza ushuru wa mazao. Mapendekezo hayo yalilenga kuimarisha manufaa kwa Sekta zote za Umma na Binafsi.

**ii. Ushuru wa Huduma Mkoa wa Morogoro:**

Hoja kuu ya mtaalam toka mradi wa ENGINE ni jinsi ya kufikia azimio linalohusu ushuru wa huduma wakati wa majadiliano ya 2017. Kupunguza kiwango cha ushuru wa huduma imekuwa ni hoja ya muda mrefu hasa kwa Sekta Binafsi. Majadiliano ya awali yalijadili suala hili lakini hapakuwa na mabadiliko yenye tija. Viongozi na Watendaji wa Mkoa, Wilaya, na Manispaa walisikiliza mapendekezo ya TCCIA na wajumbe wengine wa Sekta Binafsi lakini hawakuchukua hatua yoyote. Mtaalam alichambua takwimu za ushuru huo na kupendekeza mfumo ambao utakaokuwa na manufaa kwa Sekta ya Umma.

na Sekta Binafsi, ambao uliwasilishwa katika Mkutano wa DBC. Mtaalamu pia alimshauri Mwenyekiti wa TCCIA kuweka kando tofauti zao na viongozi wa JWT ili waweze kufanyakazi pamoja katika suala hili. Msaada huu wa kitaaluma uliwezesha maboresho ya sheria ndogo ya ushuru wa huduma.

*Kiambatisho Na. 6*

**Mfano wa sababu zinazoweza kupelekea kuahirishwa kwa Mkutano wa Baraza**

Ufuatao ni mfano halisi wa sababu zilizopelekea kuahirishwa kwa mkutano wa Baraza mnamo Juni 27, 2018, Baraza la Biashara la Mkoa wa Dar es Salaam, ambalo kwa mara ya mwisho lilikutana mwaka 2016, liliahirisha tena kutokana na kukosekana kwa akidi. Badala yake, washiriki toka Sekta ya Umma na Sekta Binafsi walitumia fursa ya kutafakari namna ya kuimarisha ufanisi wa RBC Dar es Salaa. Chini ni rejea ya majadiliano hayo:

i. Kutenga muda zaidi kwa ajili ya kazi za Mabaraza ya Biashara.
ii. Kuongeza wigo wa washiriki hasa wa ngazi ya Mkoa.
iii. Kutenga bajeti kwa ajili ya kuratibu shughuli za majadiliano Sekta Binafsi ilionyesha utayari wa kuchangia.
iv. Sababu kubwa ya kutokufanyika mikutano ya majadiliano ni ukosefu wa fedha za uratibu; Hata hivyo, Sekta Binafsi ilionyesha utayari wa kuchangia;
v. Kuongeza wigo wa ushiriki wa Sekta Binafsi kwa kuzingatia makundi mbalimbali.
vi. Kuwezesha majadiliano miongoni mwa Taasisi za Sekta Binafsi kwa ajili ya maandalizi ya majadiliano na Sekta ya Umma.

*Kiambatisho Na. 7*

## Mfano wa Bango kitita la utekelezaji wa maazimio ya mikutano

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 |
|---|---|---|---|---|---|
| **AGENDA/ MUHTASARI NAMBA** | **HOJA/ MASUALA MAKUU** | **MAAZIMIO** | **MUHUSIKA WA UTEKELEZAJI** | **MUDA WA UTEKELEZAJI** | **HATUA ZA UTEKELEZAJI** |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |

*Kiambatisho Na. 8a*

**Mfano wa Bajeti ya mkutano wa Baraza la Biashara la Wilaya**

| Baraza la Biashara la Wilaya ya Kongwa, 2018 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Na.** | **Kipengele** | **Idadi** | **Kiasi** | **Jumla** |
| 1. | **Shajala** | 100 | 1,000 | 100,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | | **100,000** |
| 2. | **Maandalizi: Mkutano wa Kamati Tendaji** | | | |
| | Viburudisho (maji na chakula) | 10 | 10,000 | 100,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | | **100,000** |
| 3. | **Gharama za Ukumbi** | | | |
| | Viburudisho (maji na chakula) | 100 | 10,000 | 1,000,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | | **1,000,000** |
| | **Jumla Kuu** | | | **1,200,000** |

*Kiambatisho Na. 8b*

**Mfano wa bajeti ya Baraza la Biashara la Mkoa**

| Baraza la Biashara Mkoa wa Morogoro, 2017 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Na.** | **Kipengele** | **Idadi** | **Kiasi** | **Jumla** |
| 1. | **Shajala** | 100 | 1,000 | 100,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | | 100,000 |
| 2. | **Maandalizi: Mkutano wa Kamati Tendaji** | | | |
| | Viburudisho (maji na chakula) | 10 | 10,000 | 100,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | | 100,000 |
| 3. | **Gharama za Ukumbi** | | | |
| | Viburudisho (maji na chakula) | 100 | 10,000 | 1,000,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | | **1,000,000** |
| | **Jumla Kuu** | | | **1,200,000** |

Baraza la Taifa la Biashara
14 Mtaa wa Jamhuri,
S. L. P. 3478,
11470 Dar es Salaam, Tanzania,
Simu: +255 22 2122984/6. Faksi: +255 22 2129433.
Barua pepe: tnbc@tnbc.go.tz
Tovuti: www.tnbc.go.tz